MWANANCHI UK 22.

MWANANCHI.CO.TZ JUMAMOSI
NOVEMBA 20, 2021
MWANANCHI

ya dhahabu

Mbegu

Louis Kolumbia, Mwananchi
lkolumbia@mwananchipapers.tz.com

Watanzania wanavyoweza kunufaika na mazao ya mifugo

Licha ya kuwa nchi ya pili barani Afrika kwa idadi ya mifugo nyuma ya Ethiopia, Tanzania haijatumia ipasavyo fursa hiyo kuuza nje bidhaa zake nje ya nchi na kuboresha uchumi wake.

Takwimu za ripoti ya sensa ya kilimo, mifugo na uvuvi ya mwaka 2020, inaonyesha kuwa Tanzania ilikuwa na ng'ombe milioni 33.9 mwaka 2020 ikilinganishwa na milioni 33.4 mwaka 2019.

Ripoti hiyo inaonyesha kuwa kulikuwa na mbuzi milioni 24 ikilinganishwa na milioni 21.29 mwaka 2019, huku kondoo wakiwa milioni 8.5 mwaka 2020 na mwaka 2019 walikuwa milioni 5.65.

Ripoti hiyo inasema wakati idadi ya kuku ikifikia milioni 87.7 kutoka milioni 83.28 mwaka 2019, nguruwe walifikia milioni 3.2 mwaka 2020 kutoka milioni 2.14 mwaka 2019.

"Sekta ya mifugo ilikuwa kwa asilimia tano mwaka 2020 na kuchangia asilimia 7.1 katika pato la Taifa (GDP), wakati mwaka 2019 ukuaji ulikuwa asilimia tano, lakini ukichangia asilimia 7.4 katika pato la Taifa," inaeleza sehemu ya ripoti hiyo.

Hata hivyo, sekta ndogo ya nyama ingeweza kuliinufaisha Taifa zaidi kupitia mauzo nje ya nchi.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alilieleza Bunge jijini Dodoma Mei mwaka huu wakati akiwasilisha bajeti ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2021/22, kuwa sekta ya nyama ilikua kwa asilimia tano na kufikia tani 738,166 kutoka tani 701,679.1.

Hata hivyo, licha ya uzalishaji huo, ni kiasi kidogo tu cha nyama kilichosafirishwa kuuzwa nje, huku wadau wakipambana kufungua masoko katika nchi za Kiarabu hasa Saudi Arabia na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

"Miaka ya nyuma usafirishaji wa nyama nje ya nchi ulifikia tani 4,000 kwa mwaka kabla ya kuathiriwa na mlipuko wa ugonjwa wa Uviko-19," alisema msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania (TMB), Dk Daniel Mushi.

Hata hivyo, alisema kuanzia mwezi Julai hadi Oktoba 2021, tani 2,000 zimesafirishwa nje ya nchi na kutoa matumaini ya kufikia tani 4,000 ifikapo Juni mwakani.

"Saudi Arabia pekee inaingiza tani 700,000 za nyama kwa mwaka, bali inayoonyesha ukubwa wa soko hilo. Watanzania wanapaswa kuchangamkia fursa hiyo ili kunufaika kiuchumi," alisema.

Uwekezaji ufanyike kwa kuboresha matunzo ya mifugo ili kuwanenepesha na kupata uzito utakaowapa manufaa ya kiuchumi, kwa mujibu wa Dk Mushi.

Fursa Saudi Arabia

Akibainisha fursa zilizopo nchini humo, Balozi wa Tanzania nchini Saudi Arabia Ally Jabair Mwadini alisema nchi hiyo ina watu milioni 34 hadi milioni 35 na kufanya iwe soko muhimu la nyama.

Alisema nchi hiyo pia inatembelewa na idadi kubwa ya watu kutoka pembe zote za dunia kila mwaka kwa ajili ya ibada za Umrah na Haji.

"Hawa wanaongeza mahitaji ya chakula ukizingatia Saudi Arabia ni nchi ya jangwa ambapo kilimo hakitoi mavuno makubwa. Hivyo basi nchi hiyo ni soko la uhakika kwa mataifa yanayoikaribia kijiografia," alisema.

Balozi wa Tanzania mjini Abu Dhabu (UAE) Mohammed Mtonga alisema licha ya fursa zinazopatikana Mashariki ya Kati, waingizaji wa bidhaa nchini humo wanapaswa kujiandaa kwa ushindani kutoka kwa wafanyabiashara wa Pakistan, Brazil Australia na India ambazo zinatawala soko.

"Wanapaswa kuwa tayari kwa kupatiwa ithibati ya uingizaji bidhaa baada ya maofisa wao kutembelea Tanzania na kukagua machinjio, kupata uelewa wa utunzaji wa mifugo na kufahamu utendaji wa mifumo ya udhibiti," alisema.

Alisema nchi za Kiarabu hazitegemei ithibati inayotolewa kwa vigezo vya Shirika la Viwango Duniani (ISO) na kubainisha kuwa wastani wa bei ya nyama nchini humo ni dirham 40 kwa kilo zaidi ya Sh 25,000.

Lakini, mkurugenzi mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara nchini (Tantrade) Latifa Khamis alisema walikuwa makini katika kutenua kampuni zitakazosafirisha nyama Saudi Arabia na UAE kwa kuzingatia uwezo na ubora ili wakakabili ushindani sokoni.

"Na sasa tunazitaka kampuni hizo zikafungue ofisi katika nchi zenye fursa ili kujiimarisha kishindani zaidi," alisema.

Alisema idadi kubwa ya maombi yaliyowasilishwa na Watanzania baada ya kubaini uwepo wa fursa katika nchi hizo wakiomba kuteuliwa kusafirisha bidhaa hiyo ni moja ya changamoto kubwa waliyokutana nayo wakati wa mchakato wa kufungua masoko ya Mashariki ya Kati.

"Wengi wao hawakuwa na uwezo, hivyo tulilazimika kuwaelimisha wajikite katika masoko ya ndani na Afrika Mashariki ingawa haikuwa rahisi kueleweka, wengine walihisi wanaonewa," alisema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, wazo la kufungua masoko ya bidhaa hizo Mashariki ya Kati lilianzishwa na taasisi yake na baadaye kuwashirikisha wawakilishi wa nchi katika maeneo husika.

> **"Miaka ya nyuma usafirishaji wa nyama nje ya nchi ulifikia tani 4,000 kwa mwaka kabla ya kuathiriwa na mlipuko wa ugonjwa wa Uviko-19."**
>
> Dk Daniel Mushi- Msajili Bodi ya Nyama Tanzania

Usafirishaji nyama nje ya nchi

Balozi Mwadini alisema walikuwa wanafanya kazi kuhakikisha zuio la kutoingiza bidhaa hiyo lililowekwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (SFDA) nchini Saudi Arabia karibu miaka 20 iliyopita kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa miguu na mdomo linaondoka.

"Nadhani hatukufanya vizuri kushughulikia suala hili maana nchi nyingine zilifanikiwa kuondoa zuio dhidi yao baada ya muda mfupi. Tunashirikiana na Wizara ya Maimbo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, TMB, Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na TanTrade kuhakikisha zuio hilo linaondolewa," alisema.

Alisema SFDA ilitembelea Tanzania mwezi Agosti mwaka huu na kukagua machinjio ya kampuni ya Tanchoice iliyopo Kibaha mkoani Pwani, Chobo na Alfachoice za jijini Mwanza na Elia Food iliyopo jijini Arusha.

Balozi Mwadini alisema ripoti ya ukaguzi ya SFDA ilionyesha haja ya kuboresha maeneo kadhaa katika machinjio yetu na kusema anaamini zuio litaondolewa mara moja baada ya maboresho kukamilika.

Mahitaji ya kuuza nyama nje

Lakini Dk Mushi alisema masoko ya nje yanahitaji nyama laini inayotafunika kwa urahisi na kwamba bidhaa kama hiyo hupatikana kwa kuchinja mifugo yenye umri mdogo iliyofikisha uzito unaoruhusiwa.

Aliwataka wadau kuona fursa ya kibiashara inayotokana na sekta hiyo ndogo na kuwekeza vya kutosha katika ufugaji wa kibiashara.

"Wanenepeshe mifugo yao na kuweka mikakati na ratiba nzuri ya uvunaji wa mifugo badala ya kufuga kwa ajili ya kupata sifa," alisema.

Masoko mapya

Kwa mujibu wa Dk Mushi, TMB inashirikiana na Tantrade kujipenyeza katika soko la China ikiwa ni jitihada za kupata masoko mapya.

Alisema kwa sasa Tanzania inasafirisha nyama kwenda nchini Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na baadhi ya nchi za kiarabu.

Malengo kufikia 2025

Dk Mushi alisema Tanzania inatarajia kusafirisha zaidi ya tani 10,000 za nyama kufikia mwaka 2025 endapo hakutakuwa na mabadiliko na mlipuko wa maradhi kama ilivyokuwa kwa Uviko-19.

"Ukame kwenye baadhi ya nchi utaipa Tanzania fursa ya kuwa msafirishaji mkubwa wa nyama kwa mauzo nje ya nchi kutakakosababishwa na kupungua uzalishaji kwenye nchi hizo," alisema.

Utolewaji wa cheti cha halal

Sheik Mkuu wa Tanzania Abubakary Zubeiry alisema wasafirishaji wa nyama kwenda nje ya nchi, wanatakiwa kupata cheti cha ithibati cha uhalali wa bidhaa za vyakula ikiwemo nyama kutoka kwenye taasisi iliyo chini ya Bakwata.

Ili kupata ithibati, kampuni zinatakiwa kuwasilisha nyaraka za usajili na barua kuthibitisha kuwapo kwa mkataba wa kusafirisha bidhaa nje ya nchi.

"Kampuni zinapaswa kuhakikisha wanapata cheti cha halal za bidhaa zao, kwani hitaji la ithibati halishii kwenye nchi za Kiarabu pekee," alisema.

Alisema ithibati hutolewa baada ya kufanyika ukaguzi wa vyanzo vya wanyama, utunzaji wake, uchinjaji na ufungashaji.

Alisema ingawa huduma hiyo inatolewa bila malipo hivi sasa, kiasi fulani cha ada kitapaswa kulipwa siku zijazo.

Scanned with CamScanner

Mazao mifugo yanavyofungua fursa za uchumi

Licha ya kuwa nchi ya pili barani Afrika kwa idadi ya mifugo nyuma ya Ethiopia, Tanzania haijatumia ipasavyo fursa hiyo kuuza nje bidhaa zake na kuboresha uchumi wake.Takwimu za ripoti ya sensa ya... UK 22

Scanned with CamScanner